SALAAM ZA MKUU WA MKOA WA ARUSHA MHE. JOHN MONGELLA KWA NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. RIDHIWANI KIKWETE WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA NNE (4) CHA SERIKALI MTANDAO FEBRUARI 8, 2024 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.

Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete; *Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

Ndugu Xavier Daudii*; Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.*

Dkt. Jasmine Tiisekwa; *Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

Mha. Benedict Ndomba; *Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

Bw. Said Seif Said; *Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,

Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali,

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo katika Kikao Kazi hiki cha Nne (4) cha Serikali Mtandao, kwani bila baraka zake tusingekuwa hapa leo.

Mhe. Naibu Waziri; Napenda kukukaribisha katika Mkoa wa Arusha, hususan katika ukumbi huu wa AICC, ambapo Kikao Kazi cha Nne (4) cha Serikali Mtandao kilichodumu kwa siku tatu (3) kinahitimishwa leo.

Napenda kuwashukuru viongozi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma na binafsi, Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali, Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na Waandishi wa Habari kwa kuwa nasi katika siku zote tatu (3) za Kikao kazi. Karibuni sana na muendelee kujisikia mpo nyumbani.

Mhe. Naibu Waziri; Naishukuru na kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kuandaa Kikao Kazi hiki na kwa ushirikiano mzuri uliopo na ofisi yangu. Wakazi wa Arusha tunafarijika sana kuona e-GA ikiendelea kuliamini jiji letu na kulichagua kuwa mwenyeji wa vikao kazi hivi kwa mara ya tatu sasa. Tunasema Asanteni sana e-GA na karibuni sana Arusha.

Mhe. Naibu Waziri; Ni matumaini yangu kuwa, katika kipindi chote cha siku tatu (3) mlizokuwepo hapa mmeweza kufurahia mandhari nzuri ya jiji la Arusha na kujionea vivutio mbalimbali vinavyopatikana hapa Arusha. Wote tunafahamu kuwa, Mkoa wa Arusha una rekodi nzuri ya kuwa na vivutio vizuri sana vya utalii hapa Tanzania na Duniani. Tuna mbuga za taifa na hifadhi za

wanyamapori, kama vile Ngorongoro, Serengeti, n.k. Nina imani kuwa mmepata fursa au mtapata fursa hiyo baada ya Kikao Kazi hiki ya kutembelea baadhi ya maeneo ya utalii na kufurahia mandhari na vivutio mbalimbali tulivyonavyo. Sambamba na utajiri wa vivutio vya utalii tulivyonavyo Arusha, pia ulinzi na usalama ni wa uhakika, na tangu mlipofika Arusha hadi leo hii mnaondoka ofisi yangu haijapokea malalamiko au matishio yoyote ya kiusalama.

Nawapongeza kwa kutembelea maeneo mbalimbali ya utalii naendelea kuwahakikisha usalama na kuwakaribisha tena wakati mwingine ili mtembelee vivutio vingi zaidi na pamoja tuweze kuinua utalii wa ndani kama ambavyo, **Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan** amekuwa akisisitiza.

Mhe. Naibu Waziri; Mkoa wa Arusha ni mmoja wa wadau wakubwa wa Serikali Mtandao kupitia kupitia taasisi mbalimbali za umma zilizopo mkoani hapa. Tumekuwa watumiaji wazuri sana wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA, katika utendaji wetu wa kazi la kila siku na katika kuwahudumia wananchi kwa wakati. Mifumo hii husaidia upatikanaji wa huduma za Serikali kwa haraka na kwa urahisi zaidi. Hii yote inatokana na jitihada kubwa inayofanya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) katika kukuza matumizi ya TEHAMA na kuhakikisha tunajenga taifa la kidijitali.

Sambamba na hilo niipongeze e-GA kwa jitihada za kuunganisha mifumo ya TEHAMA Serikalini ili iweze kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidijitali kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini – GoVESB.

Mhe. Naibu Waziri; Mkoa wa Arusha upo tayari na unaunga mkono Jitihada za Serikali Mtandao pamoja na dhamira ya dhati ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** ya kuijenga Serikali ya Kidijitali.

Nipende kutoa rai kwa Taasisi zote za Umma na Mashirika ya Serikali yaliyopo jijini Arusha, kuunga mkono utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyoidhinishwa. Tunataka Mkoa wa Arusha uwe ni mkoa wa mfano kwa mikoa mingine katika matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi, tukiwa tunaunga mkono wito wa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** wa kujenga Serikali ya Kidijitali.

Mhe. Naibu Waziri; baada ya kusema hayo machache, Nimalizie salamu zangu kwa kukushukuru tena wewe binafsi, Viongozi na wageni wote mliohudhuria hapa na ninapenda kuwakaribisha tena kutembelea jiji hili la Arusha.

Karibuni sana.

Asanteni sana kwa kunisikiliza